AOC-491 Doc. Code: EGP
Toleo la 8-14
Ukurasa wa 1 kati ya 2

Dola la Kentucky
Mahakama ya Haki *www.courts.ky.gov*

RCr 8.08, 8.10; KRS 17.169; 17.170; 532.050(1)

**MOTION TO ENTER GUILTY PLEA**

**HOJA YA KUINGIA KWENYE KUKUBALI KOSA**

Namba ya Kesi ____________________
Mahakama ____________________
Wilaya ____________________
Kitengo ____________________

DOLA LA KENTUCKY MDAI

DHIDI YA

____________________________________________ MDAIWA

Mdaiwa anakuja, ana kwa ana kwa msaada wa wakili, na kwa heshima anaiomba mahakama imruhusu kuondoa ombi la **KUKANA KOSA** na kuwasilisha ombi **la KUKIRI KOSA** kama inavyoonekana hapa chini. Katika kutetea hoja hii, Mdaiwa anaeleza kama ifuatavyo:

1. Jina langu kamili ni ____________________________________________.
Mimi ndiye mtu niliyetajwa kwenye mashtaka.

2. Maamuzi ninayotoa hayajadhurika kwa matumizi ya madawa ya kulevya, pombe au dawa zozote.

3. Nimepitia nakala ya mashtaka kumueleza wakili wangu ukweli wote ninaoufahamu kutokana na mashtaka yangu. Ninaamini ana taarifa kamili kuhusiana na kesi yangu. Tumejadiliana kwa kina na ninaelewa mashtaka na utetezi unaowezekana juu yake.

**4. Naelewa kuwa naweza "KUKANA KOSA" au "KUKIRI KOSA" kwenye mashtaka yoyote dhidi yangu.**

**5. Na zaidi ya hapo naelewa kuwa Katiba inanihakikishia haki zifuatazo:**
- **(a) Haki ya kutokutoa ushahidi dhidi yangu;**
- **(b) Haki ya kesi kuendeshwa kwa haraka na kusikilizwa hadharani na wazee wa mahakama ambapo nitawakilishwa na wakili na Jimbo litatakiwa kuthibitisha hatia yangu bila ya mashaka yoyote;**
- **(c) Haki ya kuwakabili na kuwauliza maswali mashahidi wote watakaoitwa kutoa ushahidi dhidi yangu;**
- **(d) Haki yo kuonyesha ushahidi wowote, ikiwemo kuwaita mashahidi, kwa ajili ya utetezi wangu;**
- **(e) Haki ya kukata rufaa ya kesi yangu kwenye mahakama ya juu.**

**Ninaelewa kuwa kama "NITAKIRI KOSA," nitakua nimeachana na haki hizi.**

6. Ninaelewa kwamba kama **"NITAKIRI KOSA",** mahakama inaweza kulazimika kunipa adhabu yoyote kwa mujibu wa sheria na kwamba ingawa inaweza kufikiria mapendekezo ya Jimbo, mahakama inaweza kuyakataa. Viwango vya adhabu za kisheria vinaonyeshwa katika fomu iliyoambatanishwa ya "Mapendekezo ya Jimbo baada ya Kukiri Hatia (AOC-491.1)" ambayo nimeipitia na kusaini.

7. Ninaelewa kwamba kama Mahakama itakataa maombi yangu, itapaswa kunitaarifu. Kama itatokea hivyo, ninaweza kuendelea na ombi langu la kukiri kosa na kuwa na uwezekano wa kupata adhabu kali zaidi kuliko ile niliyoitaka au naweza kuondoa ombi la kukiri kosa na kuendelea kusikiliza kesi. Zaidi ya hapo naelewa kuwa mahakama haipaswi kunihukumu kwa kosa la jinai, isipokuwa kwa kosa linaloadhibiwa kwa kifo, bila kwanza kuamuru uchunguzi unaofanyika kabla ya hukumu kufanyika. Mahakama itazingatia ripoti ya maandishi ya uchunguzi uliofanyika kabla ya hukumu kutolewa kabla haijanitaarifu kama watakubali makubaliano yaliyomo kwenye maombi.

8. Kutokana na kukubali kosa, Jimbo limekubali kupendekeza Mahakamani mashtaka na hukumu iliyotolewa katika fomu iliyoambatanishwa ya "Mapendekezo ya Jimbo baada ya Kukiri Kosa." Zaidi ya mapendekezo hayo, hakuna mtu yeyote, ikiwemo wakili wangu, aliyeniahidi kufaidika kwa aina yeyote kutokana na kukiri kosa na pia hakuna mtu yeyote aliyenilazimisha au kunitishia ili **"NIKIRI KOSA"**

9. Kwa sababu NINA **HATIA** na sijadai kuwa sina makosa, ningependa **"KUKUBALI KOSA"** kutegemeana na fomu iliyoambatanishwa ya "Mapendekezo ya Jimbo baada ya Kukiri Kosa."

FOR INFORMATIONAL PURPOSES ONLY. NOT AN OFFICIAL COURT DOCUMENT.
KWA MAJILI YA TAARIFA TU. SIO HATI RASMI YA MAHAKAMANI.

10. Ninatangaza kuwa maombi yangu ya **"KUKUBALI KOSA"** yamefanywa nikiwa huru, kwa akili yangu na kwa hiari yangu; kwamba nimewakilishwa na wakili, ambaye amenielezea kwa ukamilifu haki zangu za kikatiba, pamoja na mashtaka dhidi yangu na utetezi wake; na kwamba naelewa chanzo cha taratibu hizi na mambo yote yaliyomo katika waraka huu.

11. Naelewa kwamba kama nitatiwa hatiani kwa kosa linalohusiana na madawa ya kulevya ya methamphetamine au kosa linalohusiana na kemikali ya anhydrous ammonia iliyopo kwenye KRS Sura ya 218A, 250 au 514, itakuwa ni kinyume cha sheria kwangu kumiliki ephedrine, pseudoephedrine, phenylpropanolamine, chumvi zake au isoma za macho, au chumvi za isoma za macho miaka mitano baada ya kutiwa hatiani, kutolewa kifungoni au kuachiwa kutoka kifungo cha nje, kifungo kifupi, kuachiwa huru, au aina yoyote ya kuachiliwa kwa masharti, chochote kati ya hivi kitakachotokea baadae. KRS 218A.1446

12. Ninaelewa kwamba hukumu ya hatia ya kiwango chochote cha ubakaji, ulawiti, unyanyasaji wa kijinsia, au kunyemelea itafanyika kama maombi ya amri ya kinga ya mtu binafsi inayotolewa chini ya KRS Sura ya 456 na inaweza ikapelekea amri hiyo kutolewa.

13. Naelewa kwamba iwapo nitatiwa hatiani **kwa kosa la jinai** kwa mujibu wa Sheria Iliyofanyiwa marekebisho ya Kentucky, sampuli ya DNA yangu itachukuliwa na mtu mwenye mamlaka kwa mujibu wa KRS 17.170.

14. Naelewa kwamba mashtaka ninayotiwa hatiani leo yanaweza kustahili kufutwa kwenye rekodi kwa mujibu wa KRS Sura ya 431.

15. Naelewa kuwa kutokana na kutiwa hatiani leo hii, **ninaweza kukabiliwa na adhabu kubwa/iliyoongezwa iwapo nitakuwa na hatia na/au kupatikana na hatia katika matukio ya uhalifu katika siku za mbeleni.** Ninaelewa kuwa kama mimi siyo raia wa Marekani, naweza kufukuzwa nchini kwa mujibu wa sheria na kanuni zinazotawala Huduma za Uhamiaji na Uraia za Marekani Naelewa kikamilifu masharti ya ombi hili na wajibu wake wote uliowekwa juu yangu kwa masharti yake.

Imesainiwa katika mahakama ya wazi mbele ya wakili wangu siku ya ________________,2______.

PURPOSES ONLY. NOT AN OFFICIAL COURT DOCUMENT.
ARIFA TU. SIO HATI RASMI YA MAHAKAMA.

________________________________________
**Sahihi ya Mdaiwa.**

## UTHIBITISHO WA WAKILI

1. Kwa ufahamu wangu wote na imani yangu, mdaiwa anaelewa tuhuma zote zilizomo katika mashtaka pamoja na/au marekebisho yake. Nimejadiliana kikamilifui na mdaiwa kuhusu mashtaka na utetezi unaowezekana na ninaamini ameelewa kikamilifu mashtaka na utetezi unaowezekana. Nimepitia pamoja na mdaiwa fomu iliyoambatanishwa ya "Mapendekezo ya Jimbo baada ya Kukiri Kosa" na "Hoja ya Kuingia kwenye maombi ya "KUKIRI KOSA" iliyoacha, na ninaamini ameelewa nyaraka hizi.

2. Kwa ufahamu na imani yangu, ombi lake la **"KUKIRI KOSA"** limefanywa kwa uhuru, kwa kujua, kwa akili yake na kwa hiari yake. Nimemueleza Mdaiwa kwa ukamilifu haki zake za kikatiba na ninaamini kwamba amezielewa.

3. Ombi la "KUKIRI KOSA" kama lilivyopendekezwa na Mdaiwa liko sambamba na ushauri wangu kwake na ninapendekeza mahakamani kuwa ombi hili likubaliwe.

Imesainiwa na mimi kwenye mahakama ya wazi mbele ya Mdaiwa siku ya ________________________, 2___

________________________________________
**Wakili wa Mdaiwa**